**HALMASHURI YA WILAYA YA MKALAMA**
**UPIMAJI WA UTAMILIFU WA KIDATO CHA PILI**
**SOMO KISWAHILI**

**MUDA: 2:30** **MEI 2025**

---

**MAELEKEZO**

**1. Karatasi hii ina jumla ya sehemu tatu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10)**
**2. Jibu maswali yote**
**3. Zingatia maekekezo ya kila sehemu na kila swali**
**4. Andika mamba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi ya kujibia**

**SEHEMU A (ALAMA 15)**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Ni sentensi ipi haina kitenzi kisaidizi?
A. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa mtiifu
B. Watoto wanatakiwa kula mapema ili wawahi shuleni
C. Paka alikuwa anataka kula chakula cha Mbwa
D.Juma alikuwa anasoma kitabu Cha hadithi za mapenzi

(ii) Ni sifa ipi haitofautishi fasihi simulizi na fasihi andishi?
A. Ukubwa B. Uhifadhi C. Uwasilishaji D. Ukuaji

(iii)Ni jambo gani linalodhihirishwa upekee wa kazi fulani ya kifasihi?
A. Muundo wa kazi husika B. Jina la kazi husika
C. Wahusika wa kazi husika D. Mtindo wa kazi husika

(iv) Katika lugha ya kiswahili Kuna aina ngapi za vitenzi?
A. Mbili B. Tatu C.Sita D. Nne

(v)Kati ya sababu zifuatazo ni ipi si sahihi kuhusu matumizi ya kamusi?
A. Kujifunza lugha za kigeni B. Kusanifisha maneno mapya
C.Kujua tahajia za maneno D. Kubaini Kategoria ya maneno

(vi) Ni methali ipi inayokinzana na methali "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu"?
A. Manahodha wengi, chombo huenda mrama
B. Palipo na wengi, hapaharibiki neno
C. Kidole kimoja, hakivunji chawa
D. Fimbo ya mnyonge, ni umoja

(vii) Njia ipi ya uhifadhi wa fasihi simulizi inayoweza kupokea mabadiliko Kwa haraka kati ya hizi?.
A. Maandishi B. Kanda za video C. Kichwa D. Vinasa sauti

(viii) Fungu la sauti zinazotokea katikati au mwishoni mwa kila mstari wa ushairi huitwaje?
A. Vina B. Mizani C. Vituo D. Mistari

(ix) Ni kauli ipi iliyotumika katika uundaji wa neno " Nitamfitinia"?
A. Kutendeka B. Kutendea C. Kutendesha D. Kutendea a

(x) Barua yoyote hufuata utaratibu maalumu wa uandishi. Je, barua ya kirafiki ina vipengele vingapi?
A. Saba B.Mbili C. Sita D. Tano

| Swali | i | ii | iii | iv | v | vii | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jibu | | | | | | | | | | |

2. Oanisha Orodha A na Orodha B ili kujenga dhana sahihi. Jaza majibu yako Katika visanduku ulivyopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Kuota mizizi<br>ii. Kulea mtoto kama yai<br>iii. Chereko<br>iv. Mkono mrefu<br>v. Udongo uwahi ungali mbichi | a) Kupevuka.<br>b) Wizi<br>c) Malezi ya kudekeza .<br>d) Kutatu tatizo mapema kabla halijawa kubwa<br>e) Kukithiri<br>f.Sherehe. |

| **ORODHA A** | **i** | **ii** | **iii** | **iv** | **v** |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

**SEHEMU B ( 70 ALAMA)**

**SARUFI, MAWASILIANO, UTUMIZI WA LUGHA NA FASIHI**

3(a) Kama mtumiaji wa lugha ya kiswahili, tumia maneno yafuatayo katika sentensi kama vivumishi.
Mfano; Neno mzuri, Kijana mzuri anakula.

(i) Mwema
(ii) Stadi
(iii) Mwenyewe
(iv) Hiki
(v) Kwetu

(b) Bainisha aina za maneno yaliyo pigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

i. Amina ni msichana hodari
ii. Simama upande wa kulia
iii. Amekwenda Kwa mjomba
iv. Kijana mrefu mwembamba ametoroka shuleni
v. Lahaula! Nimechelewa tena darasani leo

4(a). Fafanua kazi za mofimu **KI** katika sentensi zifuatazo;

(i) Ukimuona atakueleza kila kitu.
(ii) Amepigana kiume
(iii) Kitabu kizuri kimechanika
(iv) Kijumba chao ni kidogo
(v) Anakitaka hiki hiki chekundu

(b). Ukiwa ni mwanafunzi wa kidato cha pili umejifunza aina za maneno ya kiswahili. Badili vitenzi vifuatavyo kuwa nomino:

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| Mfano: Kufa | Kifo |
| (i) Sifu | (i)................................... |
| (ii) Tangaza | (ii)................................. |
| (iii) Azimia | (iii)................................ |
| (iv) Zindika | (iv)................................ |
| (v) Sali | (V)................................ |

5. (a) Kama ungekuwa unashiriki moja Kwa Moja Katika mazungumzo yafuatayo yanajitokeza katika miktadha tofauti. Andika rejesta ya kila sentensi mbele ya sentensi husika

i. Wapendwa inabidi tumjue Mungu maana mshahara wa dhambi ni mauti...........
ii. Mbili asubuhi, mbili mchana na mbili jioni............
iii. Kimara, Umbungo, Mbagara, wahi twende................
iv. Boko, boko anakwenda na mpira anapiga pasi ndefu pale goooooo!! !.............
v. Mkia chapati, tia pilipili kidogo tafathari usisahau limao.................

(b) Ili lugha ya kiswahili iweze kutumika Kwa usahihi mtumiaji yeyote wa lugha azimgatie mambo matano, bainisha mambo hayo.

6. Eleza dhima tano za fasihi katika jamii ya Tanzania ya Leo

7. Andika neno moja sahihi kutokana na maelezo yafuatayo:

i. Mahali maalumu ambapo matukio ya kazi za kifasihi yanafanyika ............
ii.Tungo za fasihi simulizi zitumiazo lugha ya picha ,Tamathali za semi na ishara huitwa.........
iii. Hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli huitwa..........
iv.silabi zinazofanana zinazounda mistari ya beti za mashairi huitwa.......
V.Mbinu ya kisanaa ambayo mhusika huuliza swali ambapo jibu analifahamu huitwa.....
vi.semi zenye pande mbili zenye ukinzani ........
vii.Mstari wa mwisho katika kila ubeti huitwa......
viii.Majibazano ,mjadala au malumbano ya watu wawili au zaidi katika mtindo wa shairi .....
ix.Hadithi zinazoelezea vyanzo au chimbuko la binadamu ,Wanyama ,miti,au vituo visivyo na uhai........
x. Jumla ya mawazo, dhamira, migogoro, msimamo, mitazamo, falsafa na ujumbe katika kazi ya fasihi............

8. (a) Mwanafasihi yeyote yule lazima azitambue sifa pambanuzi za fasihi simulizi. Bainisha sifa tano za fasihi simulizi.

(b) Ukiwa mwanafunzi, toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika maana mbele ya nahau husika:

i. Ana mkono mrefu maana yake ni......................
ii. Amevaa miwani maana yake ni..........................
iv. Kupiga domo maana yake ni...............................
v. Ana macho manne maana yake ni.....................

9. Maneno yafuatayo yanatumika katika kazi za kifasihi, eleza maana ya maneno hayo:

(i) Dhamira
(ii) Fasihi
(iii) Methali
(iv) Hadithi
(v) Vigano

SEHEMU C (ALAMA 15)

10. Jifanye wewe ni Christiani mwesiga unayetarajia kufanya kumbukizi ya siku ya kuzaliwa kwako tarehe 05/07/2022. Mwandikie barua rafiki yako Justine John ukimwalika katika sherehe yako Ileje S.L.P.1024 Chunya.